Agizo La Kristo La Kutengwa (Christ's Parting Charge)

na

Ellis P. Forsman

Agizo La Kristo La Kutengwa

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 6, 2011

Agizo La Kristo La Kutengwa

Mat. 28:18-20

Mat. 28:18-20, "*Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote noliyowaamuru ninyi; na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.*"

Haya maneno ni sahihi kuitwa "*Agizo La Kristo La kutengwa*", maana hakika ni ulimwengu wote na agizo la wakati wa mwisho.

Walikuwa wanaambiwa wakina nani? Mat. 28:16, "*Na wale wanafunzi kumi na mmoja wakaenda Galilaya mpaka mlima ule aliowaagiza Yesu.*"

Tayari Tuda alikuwa amesha msaliti Yesu na tayari alikuwa amesha jinyonga, akiwaacha wale kumi na mmoja wenye idadi halisi.

Mssemo huu mkuu wa Bwana wetu inaangukia katika maeneo "*makuu*" matatu:

- Dai kuu –"*Mamlaka yote nimepewa mbinguni na duniani.*"
- Agizo kuu (sehemu 2):
- Agizo la uinjilisti – "*Basi enendeni, mkawafanye mataifa yote.*"
- Agizo la uelimishaji – "*Na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi.*"
- Uhakika mkuu – "*…na, tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.*"

Dai Kuu

"*Mamlaka yote*" (Mamlaka).

Hakuna mahali popote ambapo Yesu alidai mamlaka haya kabla ya kifo chake na ufufuo.

- Yesu akiwa na umri wa miaka 12, alikuwa mtii kwa wazazi wake. Luka 2:41-51, "*Basi wazee wake huenda Yerusalemu kila mwaka,*

wakati wa sikukuu ya Pasaka. Na alipopata umri wake miaka kumi na miwili walipanda kama ilivyokuwa desturi ya sikukuu; na walipokwisha kuzitimiza siku, wakati wa kurudi kwao, yule mtoto Yesu alibaki nyuma huko Yerusalemu, na wwazee wake walikuwa hawana habari. Nao wakadhani ya kuwa yumo katika msafara, wakaenda mwendo wa kutwa, wakawa wakimtafuta katika jamaa zao na wenzao; na walipomkosa wakarejea Yerusalemu huku wakimtafuta. Ikawa baada ya siku tatu wakamwona hekaluni, ameketi katikati ya waalimu, akiwasikiliza na kuwauliza maswali. Nao wote waliomsikia walistaajabia fahamu zake na majibu yake. Na walipomwona walishangaa, na mama yake akamwambia, mwanangu, mbona umetutenda hivi? Tazama baba yako na mimi tulikuwa tukikutafuta kwa huzuni. Akawaambia kwani kunitafuta? Hamkujua ya kuwa imenipasa kuwamo katika nyumba ya Baba yangu? Nao hawakuelewa na neno hilo alilowaambia. Akashuka pamoja nao mpaka Nazareti, naye alikuwa akiwatii; na mamaye aliyaweka hayo yote moyoni mwake."

- Wakati wake ulikuwa bado haujafika kama kijana mdogo harusini. Yoh. 2:1-10, "*Na siku ya tatu palikuwa na harusi huko Kana, mji wa Galilaya, naye mama yake Yesu alikuwapo. Yesu naye alikuwa amealikwa harusini pamoja na wanafunzi wake. Hata divai ilipowatindikia, mamaye Yesu akawaambia hawana divai. Yesu akamwambia mama tuna nini mimi nawe? Saa yangu haijawadiaa. Mamaye akawaambia watumishi, lolote atakalowaambia fanyeni. Basi kulikuwako huko mabalasi sita yam awe, nayo yamewekwa huko kwa desturi ya Wayahudi ya kutawadha kila mmoja lapata kadiri ya nzio mbili tatu. Yesu akawaambia jazilizeni mabalasi maji. Nao wakayajaziliza hata juu. Akawaambia sasa tekeni mkampelekee mkuu wa meza. Wakapeleka. Naye mkuu wa meza alipoyaonja yale maji yaliyopata kuwa divai, (wala asijue ilikotoka, lakini watumishi walijua, wale walioyateka yale maji), yule mkuu wa meza alimwita bwana arusi, kila mtu kwanza huandaa divai iliyo njema; hata watu wakiisha kunywa sana ndipo huleta iliyo dhaifu; wewe umeiweka divai iliyo njema hata sasa.*"

- Yoh. 5:19, "*Mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo amwona Baba analitenda; kwa maana yote ayatendayo yeye ndiyo ayatendayo Mwana vilevile.*"

- Yoh. 14:24, "*Mtu asiyenipenda, yeye hayashiki maneno yangu; nalo neno mnalolisikia silo langu ila ni lake Baba aliyenipeleka.*"

Kabla ya kifo chake hakuna aliyeomba kwa jina lake, lakini sasa tunapaswa kumwomba Baba kwa jina lake.

- Yoh. 16:23-24, "*…Mkimwomba Baba neno lolote atawapa kwa jina langu. Hata sasa hamkuomba neno kwa jina langu; ombeni nanyi mtapata; furaha yenu iwe timilifu.*"
- Efe. 5:20, "*Na kumshukuru Mungu Baba siku zote kwa mambo yote katika jina lake Bwana wetu Yesu Kristo.*"

Kabla ya kifo chake hakuna aliyebatizwa kwa jina lake, lakini sasa tunapaswa kubatizwa kwa jina lake.

- Mdo. 2:38, "*Petro akawaambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.*"

"*Nimepewa mamlaka yote…*"

Maneno haya yanaonyesha wakati uliotayari wakati alipopewa mamlaka haya. Alipewa lini?

Rum. 1:4, "*Na kudhihirishwa kwa uweza kuwa Mwana wa Mungu kwa jinsi ya roho ya utakatifu, kwa ufufuo wa wafu, Yesu Kristo Bwana wetu.*"

Paulo anauliza swali, na kujijibu lenyewe: Efe. 1:19-23, "*Naa ubora wa ukuu wa uweza wake ndani yetu tuaminio jinssi ulivyo; kwa kadiri ya utendaji wa nguvu za uweza wake; aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho; juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani na kila jina litajwalo wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia; akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya kanisa ambalo ndilo mwili wake ukamilifu wake anayekamilika kwa vyote katika vyote.*"

Kol. 1:18-19, "*Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani cha kanisa,, naye ni mwanzo ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote. Kwa kuwa katika yeye ilimpendeza ilimpendeza utimilifu wote ukae;*"

"Mamlaka yote nimepewa mbinguni na dunia."

Hii haimjumuishi papa wa Rumi, Joseph Smith, Bi. Baker Eddy, au mwanaume yeyote au mwanamke ambaye anaweza kudhani kwamba ukuu wa kidunia wa kanisa.

Mgawanyiko wa kidini leo haupo katika kutafsiri kama ilivyo katika kukosa heshima kwa mamlaka sahihi – mamlaka ya Yesu Kristo.

Agizo kuu. Iko katika pande mbili: inaita watu katika uinjilisti na kuelimisha

Agizo la uinjilisti.

"Basi enendeni..."

Kwa sababu Yesu alikuwa na mamlaka yote, alikuwa sahihi kuwaambia, "*Enendeni*".

Kama mtu amekuja nyumbani kwako na kuwaambia watoto wako waende kuosha vyombo, au waende wakamwage uchafu, kwa mamlaka yapi atakuwa anafanya haya. Hakuna.

Kwa sababu Kristo ana mamlaka yote aliyopewa na Baba yake, ana haki ya kutoa agizo lolote analotaka.

"...na kufundisha mataifa yote." (Kutengeneza wanafunzi).

Chini ya Agano Jipya, mwanafunzi ni Mkristo.

Mdo. 11:26, "*Hata alipokwisha kumwona akamleta Antiokia. Ikawa kwa muda wa mwaka mzima wakakusanyika pamoja na kanisa na kuwafundisha watu wengi. Na wanafunzi waliitwa Wakristo kwanza hapo Antiokia.*"

Hivyo, "*Enendeni na kuwafanya Wakristo.*"

Katika agizo kuu tunajifunza jinsi ya kufanyika Wakristo.

- **Amini.** Marko 16:15-16, "*Akawaambia enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri injili kwa kila kiumbe aaminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini atahukumiwa.*"
- **Tubu.** Luka 24:46-47, "*Akawambia ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu; na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu.*"
- **Kiri.** Rum. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu.*"

- **Ubatizo.** Mat. 28:19, "*Basi enendeni mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu;" Marko 16:16, "Aaminiye na kubatizwa ataokoka, asiyeamini atahukumiwa.*"

"...mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu."

Hii inamanisha kubatiza kwa mamlaka yao yaliyounganishwa pamoja.

Hiki ndio kitu pekee ambacho kinapaswa kufanya kwa jina la vitatu vyote.

Yoh. 3:5, "*Yesu akajibu, amin, amin, nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuungia ufalme wa Mungu.*"

Agizo la kuelimisha.

"Mkiwafundisha kuyashika yote..."

Hiyo ni, kuwafundisha waumini ambao tayari wamesha batizwa. Wakristo wanapaswa kufaham cha kufanya ili kuwaweka wakiwa kwenye wokovu, kadiri ambavyo mwenye dhambi anavyopaswa kujua anachopaswa kufanya ili aokolewe kutoka katika (mambo ya zamani) dhambi.

Nyaraka 21 katika Agano Jipya wameandikiwa Wakristo; hivyo, kuna hotuba nyingi kwa ajili ya kanisa kuliko kwa wenye dhambi.

Hivyo basi, tunapaswa kila wakati kuendelea kuwafundisha Wakristo. 1 Tim. 4:6, "*Uwakumbushe ndugu mambo hayo, nawe utakuwa mtumishi mwema wa Kristo Yesu, na mvoevu wa maneno ya imani na mafundisho mazuri yale uliyoyafuata.*"

Kwa nini hili ni muhimu? Ili kwamba kanisa liweze "*kuwa imara*" katika huduma ya Bwana.

- Mdo. 2:42, "*Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali.*"
- Efe. 4:14, "*Ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, kwa ujanja, tukizifuata njiaa za udanganyifu.*"
- 2 Pet. 2:20-21, "*Kwa maana wale waliokwisha kuyakimbia machafu ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo, kama wakinaswa tena na kushindwa, hali yao ya mwisho imekuwa*

mbaya kuliko ile ya kwanza. Maana ingekuwa heri kwao kama wasingaliijua njia ya haki, kuliko kuijua kisha kuiacha ile amri takatifu waliopewa."

"...kuyashika yote niliyowaamuru."

- Mdo. 20:20, "*Ya kuwa sikujiepusha katika kuwatangazia neno lolote liwezalo kuwafaa bali naliwafundisha waziwazi, na nyumba kwa nyumba,*"
- Mdo. 20:26-27, "*Kwa hiyo nawashuhudia wote siku hii ya leo ya kuwa mimi sina hatia kwa damu ya mtu awaye yote. Kwa maana sikujiepusha na kuwahubiria habari ya kusudi lote la Mungu.*"

Hakuna kisicho muhimu katika mafundisho ya Kristo, na hakuna umuhimu nje ya mafundisho yake. 2 Yoh. 1:9, "*Kila apitaye cheo wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu. Yeye adumuye katika mafundisho hayo, huyo ana Baba na Mwana pia.*"

Uhakika mkuu. Ahadi hii iko mara tatu.

Ahadi ya uwepo binafsi – "*Niko pamoja anyi.*"

Siyo muwakilishi wangu, lakini, "*Mimi*", binafsi. Heb. 13:5, "*Msiwe na tabia ya kupenda fedha; mwe radhi na vitu mlivyo navyo; kwa kuwa yeye mwenyewe amesema, sitakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa.*"

Hatatuacha , bali sisi tunaweza kumwacha.

- 1 Tim. 4:1, "*Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidaanganyazo, na mafundisho ya mashetani;*"
- 2 Pet. 2:19-22, "*Wakiwaahidia uhuru, nao wenyewe ni watumwa wa uharibifu, maana mtu akishindwa na mtu huwa mtumwa wa mtu yule. Kwa maana wale waliokwisha kuyakimbia machafu ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo, kama wakinaswa tena na kushindwa, hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza. Maana ingekuwa heri kwao kama wasingaliijua njia ya haki, kuliko kuijua kisha kuiachaa ile amri takatifu waliopewa. Lakini imetukia kwao sawasawa na ile mithali ya kweli, mbwa ameyarudia matapiko yake mwenyewe, na nguruwe aliyeoshwa amerudi kugaagaa matopeni.*"
- Mat. 18:20, "*Kwa kuwa walipo wawili watatu wamekussanyika kwa jina langu, nami nipo papo hapo katikati yao.*"

- Yoh. 12:26, "*…nilipo mimi, ndipo mtumishi wangu atakapo kuwapo…*"

Uwepo wa kushikamana – "*Siku zote.*"

Neno hili "*siku zote*" linamtenganisha na kila mwalimu ambaye ulimwengu umewahi kumfaham. Heb. 13:5-6, "*Msiwe na tabia ya kupenda fedha; mwe radhi na vitu mlivyo navyo; kwa kuwa yeye mwenyewe amesemaa, sitakupungukia kabisa. Hata twathubutu kusema, Bwana ndiye anisaidiaye, sitaogoapa;*"

Ushindi uliopo – "*…hata ukamilifu wa dahari.*"

Wakati wote, hadi katika mwisho wa dunia. Kwa vile ujumbe wa injili unapaswa kuhubiriwa, na katika kulihubiri Bwana ameahidi kuwa pamoja nasi hadi katika ukamilifu wa dahari, alafu katika siku zote hizo injili inapaswa kuendelea kuhubiriwa.

1 Pet. 1:25, "*Bali neno la Bwana hudumu hata milele. Naa neno hilo ni neno lile jema lililohubiriwa kwenu.*"

Karne zimekwenda, falme zimenyanyuka na kuanguka, mabadiliko yasiyohesabika imefanywa katika dunia hii toka dunia hii ilipotamkwa na Bwana wetu, bado injili ni ile ile.

Wakati mwingine tunaweza kuwa wenye mabadiliko wanaolia, "Tunahitaji injili mpya na tofauti kwa ajili ya kizazi kipya."

Dunia haihitaji injili mpya tenaa isipokuwa inahitaji jua jipya ili liweze kuleta mwanga, au ulimwengu mpya ambayo wataishi.

Mungu alitengeneza jua, hewa, maji, na dunia, na vitu hivi vyote vitakidhi mahitaji ya mtu mwenye mwili hadi mwisho wa dunia.

Mungu huyo huyo alitupatia injili ya Yesu Kristo, na itatosha kukidhi mahitaji ya wanadamu waliopotea hadi Kristo atakapompa Baba ufalme.

Haishangazi Yuda akaandika katika Yuda 1:3 kuhusu "*imani waliopewa watakatifu mara moja tu.*"

Hata kama Yesu ameshapaa katika mkono wa kiume wa Mungu, uwepo wake ulioshikamana bado una linda, fariji, na kuwabariki wateule wake. Yesu kwa Paulo kwa Wakorintho, Mdo. 18:10, "*Kwa kuwa mimi ni pamoja nawe, wala hapana mtu atakayekushambulia ili kukudhru;k kwa maana mimi nina watu wengi katika mji huu.*"

- Yuko pamoja nasi tunapozunguka meza ya Bwana. 1 Kor. 11:26, "*Maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo.*"

- Yuko pamoja nasi tunapoomba. Heb. 7:25, "*Naye kwa sababu hii aweza kuwaokoa kabisa wao wamjiao Mungu kwa yeye; maana yu hai siku zote ili awaombee.*"

- Yuko pamoja nasi tunapomuimbia nyimbo za sifa. Heb. 13:15, "*Basi kwa njia yake yeye na tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima, yaani tunda la midomo iliungamayo jina lake.*"

Yuko pamoja nasi tunapojaribiwa. 1 Kor. 10:13, "*Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa iliyo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili.*" 2 Pet. 2:9, "*Basi Bwana ajua kuwaokoa watauwa na majaribu, na kuwaweka wasio haki katika hali ya adhabu hata siku ya hukumu.*"

- Atakuwa pamoja nasi tunakuja katika bonde la mauti kutoa usalama ili tuvuke katika bonde la kutenganisha. Zab. 23:4, "*Naam, nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya; kwa maana wewe upo pamoja nami, gongo lako na fimbo yako vyanifariji.*"

Hitimisho

Unapokuja katika bonde la mauti unaweza kudai Bwana ndiye kiongozi wako?

Atakuwa pale kukutia nguvu na kukuongoza katika uzima wa milele usiokuwa na mwisho?